

# SALAA



UWONGOZI KWA WAIISLAMU WE PYA

# SALAA

**Uwongozi kwa Waislamu Wepya**

**Muharram 1441 / September 2019**

Haki zote Zimehifadhiwa

Kimetungwa na Kuchapishwa na



**مركز التعريف بالإسلام**  
**Islamic Information Center**  
Sultan Qaboos Grand Mosque, Muscat  
Sultanate of Oman  
Telefax. (968) 2450 5170  
[www.iicoman.om](http://www.iicoman.om)



# **YALIYOMO**

Dibaji .....	1
<i>Mlango wa 1. Utangulizi</i> .....	2
<i>Mlango wa 2. Tahara (Usafi wa kiibada)</i> .....	4
► Unajisi wa nje	
► Unajisi wa kiibada	
<i>Mlango wa 3. Wudhuu (Kutawadha)</i> .....	8
► Wudhuu	
► Tayammum	
► Mambo yanayotenguwa Wudhuu	
<i>Mlango wa 4. Salaa</i> .....	16
► Aina za Salaa	
► Nyakati za Salaa	
► Vipi Kusali	
► Vitendo vinavyo haribu Salaa	
<i>Mlango wa 5. Salaa ya Jamaa</i> .....	21
<i>Mlango wa 6. Mambo Yanayohusu Wanawake</i> .....	25
<i>Mlango wa 7. Tafauti katika Salaa baina ya wanavyuoni katika shariya za Kiislamu</i> .....	27
<i>Mlango wa 8. Mambo mabalimbali na Dasturi</i> .....	29
<i>Mlango wa 9. Taratibu ya Salaa</i> .....	35
<i>Mlango wa 10. Orodha ya Maneno</i> .....	46

# Dibaji

---

Salaa ina umuhimu mkubwa katika ibada ya Kiislaamu. Mtume Muhammad, salaa na amani za Mola wetu ziwe juu yake, amesema: "Kila kitu kina nguzo na nguzo ya dini ni Salaa."<sup>1</sup> Vilevile amesema: "Jambo la kwanza tutakalo hesabiwa Siku ya Hesabu ni Salaa zetu."<sup>2</sup>

Salaa zetu za kila siku ni njia ya kudumisha utambuzi na fikira zetu juu ya Allah katika maisha yetu ya kila siku. Utambuzi huu na fikira hii juu ya Allah ndio yanayotukinga na maovu yote, kama tusomavyo katika Qur'an:

وَأَقِمِ الصَّلَاةَ ۖ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ

*Simamisha Salaa, hakika Salaa inazuilia mambo machafu  
na maovu. (Qur'an 29:45)*

Na vilevile utambuzi wetu na fikira zetu juu ya Allah ndio zinazo tukumbusha wajibu wetu kwa Allah na wajibu wetu kwa viumbe kwa jumla. Kwa hivyo umuhimu wa Salaa katika Uislamu hauwezi kutiliwa nguvu zaidi ya hivi. Na jambo la mwanzo kwa yule aliyejiunga katika Uislamu ni kujifunza Salaa. Kitabu hichi kinetengenezwa ili kumpa yule aliyejiunga katika Uislamu, mambo muhimu ya Salaa ambayo anayahitajia ili aweze kuanza kutekeleza hii nguzo muhimu ya Uislamu. Kwa hivyo yule aliyejiunga katika Uislamu anahimizwa (na anatakiwa) kutafuta ilimu zaidi ya maelekezo ya ibada hii na namna nyengine za ibada katika Uislamu.

Kitabu hichi kinaelezeya sharti na yakufanywa kabla ya Salaa, Salaa tano za faridha, Salaa ya Ijumaa na Salaa nyenginezo za kuongeza amabazo zinajulikana kwa lugha ya Kiarabu *Sunnah*. Hazikutajwa humu Salaa nyenginezo kama Tarawehe ya Mwezi wa Ramadhani, Salaa ya maiti, Salaa za Idi mbili na nyenginezo ambazo huweza kupatikana katika vitabu vya Salaa vyengine.

---

1 Hadithi hii ya Mtume imeandikwa na ar-Rabi'i

2 Hadithi hii ya Mtume imeandikwa na at-Tirmidhi



# Mlango wa 1 - Utangulizi

1. Salaa ni nguzo ya pili katika Uislamu na imeamrishwa na Allah (swt)<sup>3</sup> katika aya mbalimbali za Qur'an. Kwa mfano anasema Allah (swt):

فَأَقِمُوا الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوفًا

*Simamisheni Salaa kama dasturi. Kwani hakika Salaa kwa  
Waumini ni faridha iliyo wekewa nyakati maalumu.*

*(Qur'an 4:103)*

Mtume Muhammad (saw)<sup>4</sup> amesema:

*Kitu kinacho mpambanuwa muumini na yule asiye muumini ni  
Salaa, kwani yeyote anayeiacha amekufuru.*

*(Imeandikwa na Ar-Rabi'i, At-Tirmidhiy, Ahmed, Ibn Majah na wengineo)*

2. Salaa imelazimishwa kwa kila Muislamu aliyebalighi mwenye akili zake timamu, kwa wanaume na wanawake. Mtume (saw) amesema kuwa mtoto hawajibiki mpaka abalighi, na mwenye wazimu mpaka apone wazimu.<sup>5</sup>
3. Muislamu anapaswa kusali Salaa za faridha mara tano kwa kila siku katika nyakati zake zilizo amuriwa. (angalia Mlango wa Nne kuhusu nyakati za Salaa).
4. Wakati unapotaka kusali, unatakiwa kwanza uwe umo katika usafi kamili wa kiibada. (Usafi huu unaitwa Tahara, angalia Mlango wa Pili kuhusu Tahara).
5. Pale unapokuwa umo katika hali ya Tahara, unatakiwa utie Wudhuu (utawadhe) ili uweze kusali. (Angalia Mlango wa Tatu kuhusu Wudhuu).

<sup>3</sup> Pale tunapolitaja jina la Allah tunasema 'Subhanahu wa Ta'ala' (swt), maana yake 'Mwenye sifa kuu na Mtukufu'.

<sup>4</sup> Pale tunapolitaja jina la Mtume tunasema Salla Allahu Alayhi wa Sallam, (saw).

<sup>5</sup> Hadithi hii ya Mtume (saw) imeandikwa na Ahmed, Abu Dawud, Ibn Maja na wengineo.



- Katika Uislamu kila kitendo kinalipwa kwa makusudio yake (*Niyyah*). Kwa hivyo kabla ya kufanya vitendo hivi vya *Tahara*, *Wudhuu* na *Salaa*, anatakiwa mtu atie nia kwa makusudio yake katika moyo wake kuwa anataka kufanya vitendo hivi kwa kumtii Allah (swt).
- Salaa husaliwa kwa lugha ya Kiarabu, kwa sababu ndani yake kuna kusoma Qur'an ambayo ni kwa Kiarabu. Mtume (saw) alipoongozwa na Malaika Jibril namna ya kusali ilikuwa ni kwa lugha ya Kiarabu. Kwa hivyo kusali kwa lugha nyengine kutaondoa maana ya ndani iliyo kusudiwa na utakatifu na umuhimu uliomo ndani ya maneno ya Salaa.

وَجَاهُوا فِي اللَّهِ حَقًّا جِهَادَةً هُوَ أَجْبَابُكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي  
 الَّدِينِ مِنْ حَرَجٍ مَّلَأَهُ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ هُوَ سَمَّانُكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ  
 قَبْلُ وَفِي هَذَا لَيْكُونُ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ  
 عَلَى النَّاسِ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَاعْثُرُوا الْزَكُوَةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ  
 هُوَ مَوْلَكُكُمْ فَنِعْمَ الْمَوْلَى وَنَعْمَ الْنَّصِيرُ

Na fanyeni juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama inavyo stahiki jihadi yake. Yeye amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteeni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur'ani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu. Basi shikeni Sala na toeni Zaka na shikamaneni na Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mlinzi wenu, Mlinzi bora kabisa, na Msaidizi bora kabisa. (Qur'an 22:78)



## Mlango wa 2 - Tahara (Usafi wa kiibada)

Kabla ya kusali, Muislamu anatakiwa ajisafishe na unajisi wa nje na unajisi wa kiibada, (*Najasa na Hadath al-Akbar* kwa Kiarabu).

Allah (swt) anasema:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْتَّوَابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

*Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao tubu na huwapenda  
wanao jitakasa. (Qur'an 2:222)*

Mtume Muhammad (saw) amesema:

*Ufunguo wa Salaa ni kujitakasa*

*(Imeandikwa na at-Tirmidhiy, Abu Dawud na Ibn Majah)*

### 1. Unajisi wa nje (Najasa)

Yafuatayo ni lazima yasafishwe katika mwili, nguo na pahala unapo sali, kabla ya kusali.

- a. Mkojo; ikiwa ni wa binadamu au mnyama.
- b. Choo cha binadamu na wanyama, isipokuwa kile cha wanyama na ndege ambao wameruhusiwa kuliwa katika Uislamu.
- c. Damu ya namna yoyote isipokuwa damu ya samaki au ya nyama inayotoka wakati unapotayarisha nyama hizi.
- d. Matapishi.
- e. Umaji au chakula kinachotoka tumboni mpaka rohoni kikarudi tena, yaani macheuzi.
- f. *Manii* yanayotoka wakati wa kitendo cha ndoa au kwa kuota usingizini au hata kwa kujichezea.
- g. Maji mepesi yanayotoka uumeni wakati wa kuchazeana mume na mke kabla ya kitendo cha ndoa. (Kwa lugha ya Kiarabu yanaitwa *Madhee*).
- h. Maji mepesi yanayotoka baada ya mkojo. (Kwa lugha ya Kiarabu yanaitwa *Wadee*).



## **Kusafisha Unajisi wa nje (Najasa):**

Unajisi wa nje, ikiwa katika kiwiliwili au nguoni au popote unaweza kusafishwa kwa kukosha kwa maji. Ikiwa uchafu unaotokana na mbwa, (mkojo, mate au choo) ni lazima kukosha vizuri kwa maji mara saba, na mara moja katika hizo iwe kwa mchanga au udongo safi. Katika hali zote, ikiwa kumebaki harufu kidogo au doa baada ya kusafisha, basi hapana neno.

## **2. Unajisi wa kiibada, (*Hadath al-Akbar*)**

Mtu anakuwa yumo katika unajisi wa kiibada akiwa katika hali hizi tatu zifuatazo:

- a. Hali ya kuwa umo katika *Janaba*: Baada ya kitendo cha ndoa au kutokwa kwa *manii* ikiwa umacho au kwa kuota usingizini.
- b. Hali ya *Hedhi*: Wakati mwanamke yumo katika ada yake ya mwezi.
- c. Hali ya *Nifaas*: Wakati mwanamke mzazi anatoka damu ya baada ya uzazi (hii dasturi inakuwa siku 40).

## **Kujisafisha Unajisi wa kiibada, (*Hadath al-Akbar*)**

Kujisafisha unajisi wa kiibada ni kwa kukoga (kwa lugha ya Kiarabu inaitwa *Ghusul*). Unatakiwa kukoga mwili mzima kama ifuatavyo:

- a. Tia niya katika moyo wako ya kukoga ili kujisafisha na unajisi wa kiibada.
- b. Jaribu kukojoa (kwa kufanya hivi unasafisha Manii yaliyobaki katika njia ya mkojo).
- c. Kosha sehemu zako za siri kutoka kitovu mpaka magoti na sehemu zozote zilizo enea uchafu.
- d. Sema ‘*Bismillah*’ (Maana yake ‘Kwajina la Allah).
- e. Tia *Wudhuu* kama unapotaka kusali. (tazama Mlango wa Tatu).
- f. Kosha kwa maji vizuri mwili wako kamili, kuanzia juu kabla ya chini, tena kulia kabla ya kushoto.



## **Mambo Muhimu kuhusu Tahara**

- a. Mtu anayekuwa hana *Tahara* (yaani si *Tahir*) haruhusiwi kutenda haya yafuatayo:
  - 1. Kusali.
  - 2. Kufunga.
  - 3. Kushika msahafu (Qur'an) au kuusoma.
  - 4. Kuingia mskitini.
- b. Yeyote atakaye ingja katika Uislamu mara tu anatakiwa akoge (*Ghusul*).
- c. Ikiwa mtu haijuwi *Najasa* imempata wapi katika mwili wake, basi kutoa wasiwasi anatakiwa akoge (*Ghusul*) ili kuusafisha mwili wote.



يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوْا وُجُوهُكُمْ وَأَيْدِيکُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُّبًا فَاطَّهِرُوْا وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَى أَوْ عَلَى سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِنْكُمْ مِنَ الْغَابِطِ أَوْ لِمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجْدُوا مَاءً فَتَيَمِّمُوْا صَعِيْدا طَيِّبا فَامْسَحُوا بُوْجُوهُكُمْ وَأَيْدِيکُمْ مِنْهُ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ حَرَاجٍ وَلَكِنْ يُرِيدُ لِيُظْهِرَكُمْ وَلِيُتَمِّمَ نِعْمَةُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشَكُّرُونَ

*Enyi mlion amini! Mnapo simama kwa ajili ya Salaa osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni kwa vumbi lililo safi, na mpanguse nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru. (Qur'an 5:6)*

عن أبي هريرة رضي الله عنه أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: «الصلوات الخمس، والجمعة إلى الجمعة، كفارة لما بينهن، ما لم تغش الكبائر»

**Abu Hurairah (Radhi za Allah ziwe juuyake) amesimulia:**

*Mtume wa Allah amesema: Salaa tano za kila siku na Salaa ya Ijumaa mpaka Ijumaa ya pili hufidia madhambi madogo aliyo yafanya mja, kwa shuruti ya kuepuka na madhambi makubwa.*

**(Imeandikwa na Muslim)**



## Mlango wa 3 - Wudhuu

Yeyote aliyejikuwa Tahir anatakiwa kwanza kutia *Wudhuu* ili kuweza kusali. Mlango huu umegawika sehemu tatu: 1. *Wudhuu*, 2. *Tayammum*, na 3. Yale yanayo tenguwa *Wudhuu*.

### 1. Wudhuu

*Wudhuu* humuandaa Muislamu kiwiliwili na kiroho ili kumkabili Allah katika Salaa. Inahitajika kukosha baadhi ya viungo vya mwili kwa utaratibu ulio amrishwa na Allah pamoja na Mtume Wake (saw). Allah anasema katika Qur'an:

يَأَيُّهَا الْذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قَمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهُكُمْ وَأَيْدِيکُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ  
وَامْسَحُوا بِرُءُوسُكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ

*Enyi mlio amini! Mnapo simama kwa ajili ya Salaa osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. (Qur'an 5:6)*

Mtume (saw) amesema:

*Salaa ya mtu asiyetia Wudhuu haithibiti.*

*(Imeandikwa na Ibn Majah, Abu Dawud na wengineo)*

### Vipi kutia Wudhuu (kutawadha)

Kwanza tia niya katika moyo wako ya kujitakasa na uchafu mwilini kwa kutia Wudhuu. Baadae sema:

بِسْمِ اللَّهِ

*(Bismillah, maana yake 'Kwa jina la Allah')*

Sasa unatakiwa kufuata hatuwa 8 kama zilivyo elezewa katika kurasa mbili zifuatazo.





①

Kosha mara tatu viganja vyako viwili mpaka kwenye vifundo. Hakikisha maji yanafika kote na baina ya vidole.



②

Kwa kutumia kiganja chako cha kulia teka maji uyatie mdomoni na usukutuve vizuri na ujaribu kuyafikisha mpaka kooni. Fanya haya mara tatu..



③

Baadae teka maji kwa kiganja chako cha kulia uyavute katika pua yako kama uwezavyo ili kusafisha tundu za pua. Pangusa mafua kwa mkono wako wa kushoto. Fanya haya mara tatu.



④

Kwa kutumia mikono yako miwili (viganja) kosha uso wako mara tatu, kuanzia kipaji cha uso mpaka kidevuni na ufikishe maji kwa kutumia mikono yako mpaka masikioni.





5

Kosha mkono wako mpaka kiwiko cha mkono, na baina ya vidole mara tatu. Anza mkono wa kulia baadae mkono wa kushoto.



6

Pangusa mara moja kichwa chako kwa mikono yako miwili iliyomaji, kuanzia mbele mpaka nyuma..



7

Pangusa ndani ya masikio kwa kutumia vidole vilivyo vimaji, vilevile pangusa nyuma ya masikio kwa kutumia vidole gumba vilivyo vimaji. Fanya haya mara moja.



8

Kosha mguu mpaka kifundoni mara tatu, kwa kuhakikisha unasafisha baina ya vidole mpaka nyayo. Anza mguu wa kulia na baadae wa kushoto.



Hatuwa hizi nane zinamaliza kutia Wudhuu. Hapa unaweza kuomba dua hii:

أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهُدُ أَنَّ مُحَمَّداً رَسُولُ اللَّهِ  
اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَابِينَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ

**Ash'hadu an laa ilaha illa Llah wa ash'hadu anna Muhammadan rasuulu Llah. Allahumma j'alni mina ttawwabin wa j'alni mina lmutatahirin.**

*Nashuhudia kuwa hapana mungu wa kuabudiwa isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mjambe wake. Ewe Mola nije alie mionganoni mwa wale wanao tubia na mionganoni mwa wale walio jitakasa nafsi zao.*

### Mambo muhimu katika Wudhuu

- a. Hakikisha kuwa maji yanafika sehemu zote zinazo takiwa kukoshwa. Lakini jaribu usipoteze maji kwa kutaka kukosha zaidi ya mara tatu.
- b. Wudhuu hautimii ukiwa umefanywa juu ya urembo uliotiwa ambao unazuwia maji kufikia kwenye ngozi.
- c. Ikiwa mtu anatokwa damu mfululizo kwenye kijaraha au puanini, anatakiwa azibe ili kuziwia damu na aendelee na Wudhuu wake na kusali. Haya pia yanamhusu mwanamke ambaye anatokwa na damu nje ya siku zake za ada.
- d. Wudhuu unatakiwa utiwe kwa maji yaliyo safi, kama ya mferejini, maji ya mvua, maji ya baharini na maji yaliyo toka kwenye theluji au barafu. Maji yaliyo changanywa na kitu kisafi kama sabuni, zaafarani, mauwa na kadhalika basi yanafaa kutumika.
- e. Wudhuu haufai kutiwa kwa maji yaliyo ingia uchafu au chochote kitachoharibu ladha yake, rangi au harufu.



## 2. Tayammum

*Tayammum* ni njia ya kujisafisha najasa, unajisi wa kiibada na kutia Wudhuu, kwa kutumia mchanga au vumbi safi. *Tayammum* hufanyikana kwa hali hizi:

- Panapokuwa hakuna maji. Allah anasema katika Qur'an:

وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ الْغَابِطِ أَوْ لَمْسَتُمُ الْنِسَاءَ فَلَا مُهِاجِرَةٌ مَّا إِذْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمِّمُوا صَعِيدًا طَيْبًا فَامْسَحُوا بُوْجُو هُكْمٌ وَأَيْدِيكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُوا غَفُورًا

*Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake (kwa kitendo cha ndoa) na msipate maji, basi ukusudieni mchanga safi, mpanguse nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni msamehevu na Mwenye kughufiria. (Qur'an 4:43)*

- Kutokuweza kutumia maji kwa sababu ya baridi kali, kuogopa kuzidisha ugonjwa au kuchelewesha kupona ugonjwa na kadhalika.
- Maji yaliyopo yanahitajiwa kwa kunywa.



Unapo taka kutayamam kwanza tia nia, tena sema *Bismillah* na ufuate utaratibu ufuatao:

**1:** Piga mchanga au udongo kwa viganja vyakao miwili, kumuta viganja vyakao halafu pangusa uso wako mara moja kama unavyo tawadha.



**2:** Piga mchanga au udongo kwa viganja vyakao mara ya pili, kumuta na baadae kwa kutumia kiganja cha kushoto pangusa kiganja cha kulia mbele na nyuma mpaka kwenye kifundo na vidole. Baadae kwa kiganja cha kulia pangusa kiganja cha kushoto kama mwanzo.



## *Hadithi kuhusu Wudhuu*

عَنْ ابْنِ عُمَرَ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ قَالَ: مَنْ تَوَضَّأَ عَلَى طُهْرٍ كَتَبَ اللَّهُ لَهُ بِهِ عَشْرَ حَسَنَاتٍ

Imeelezewa katika hadithi kutokana na Ibn Umar kuwa Mtume (saw) amesema: yejote anayetia Wudhuu naye yumo kati hali ya tahara, Allah humuandikia thawabu za vitendo vyema kumi. (Imeandikwa na at-Tirmidhi)

حَدَّثَنَا عَمْرُ بْنُ سَعِيدَ بْنُ الْعَاصِ، قَالَ كُنْتُ عِنْدَ عُثْمَانَ فَدَعَاهُ بَطْهُورٌ فَقَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ "مَا مِنْ امْرٍ مُسْلِمٍ تَحْضُرُهُ صَلَاةً مَكْتُوبَةً فَيَحْسِنُ وُضُوءَهَا وَخُشُوعَهَا وَرُكُوعَهَا إِلَّا كَانَتْ كَفَارَةً لِمَا قَبْلَهَا مِنَ الذُّنُوبِ مَا لَمْ يُؤْتِ كَبِيرَةً وَذِلِّكَ الدَّهْرُ كُلُّهُ".

'Amr ibn Sa'id ibn al-'As ameeelzea: Nilikuwa pamoja na Uthman, akaomba maji ya kutawadhi, akasema: Nilimsikia Mtume wa Allah (saw) akisema: Unapofika wakati wa Salaa, Muislamu yejote akatia Wudhuu vizuri baadae kusali kwa unyenyekevu atafutiwa dhambi zake zilizo pita, isipokuwa madhambi makubwa; na haya ni kwa wakati wote. (Imeandikwa na Muslim)

رَأَى رَسُولُ اللَّهِ - صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - رَجُلًا يَتَوَضَّأُ فَقَالَ "لَا تُسْرِفْ لَا تُسْرِفْ"

Mtume wa Allah alimuona mtu anatawadha akamwambia: "Usipite kiyasi, usipite kiyasi (katika kutumia maji)."

(Imeandikwa na Ibn Majah)



### **3. Vitendo vinavyo haribu Wudhuu**

Yeyote aliye tia *Wudhuu* anakuwa yumo katika usafi wa mwili na roho kusimama mbela ya Allah katika Salaa. Yafuatayo yanatengua ule usafi na huwa ni lazima kutia *Wudhuu* tena:

1. Kutokwa na chochote kwenye sehemu za siri, (mkojo, choo, upepo, manii na umaji wowote).
2. Usingizi unao ondoa fahamu.
3. Kuondokewa na fahamu kwa sababu yoyote.
4. Kugusa sehemu za siri kwa mkono bila ya kinga.
5. Kugusa *Najasa* (angalia Mlango wa Pili, namba 1).
6. Kutokwa na damu (vilevile angalia “Mambo muhimu katika Wudhuu” namba **c**, hapo juu).
7. Kutapika na kucheuwa.
8. Kufanya vitendo visivyo vyta halali katika Uislamu kama kusengenya, kusema uwongo, na kadhalika.




# Mlango wa 4 - Salaa

Mlango huu umegawika sehemu nne: 1. Namna za Salaa, 2. Nyakati za Salaa, 3. Vipi kusali, 4. Vitendo vinavyo tenguwa Salaa.

## 1. Namna za Salaa

Katika Salaa kuna harakati zifuatazo:



Kusimama, kuinama (Ruku'u) na kusujudu mara mbili huwa ndiyo Raka'a moja. Kuna namana nyingi za Salaa na kila moja ina idadi mbalimbali za Raka'a. Ifuatayo ni orodha ya Salaa na Raka'a zake.



### **Salaa za lazima za kila siku, (*Faridha*)**

	<b>Salaa</b>	<b>Raka'a</b>
1	Salaa ya Alfajiri ( <i>Fajr</i> )	2
2	Salaa ya Adhuhuri ( <i>Dhuhr</i> )	4
3	Salaa ya Alasirri ( <i>Asr</i> )	4
4	Salaa ya Magharibi ( <i>Maghrib</i> )	3
5	Salaa ya Isha ( <i>Isha</i> )	4
6	Salaa ya Ijumaa	2

### **Salaa za nyongeza (*Sunna*)**

	<b>Salaa</b>	<b>Raka'a</b>
1	Kabla ya Salaa ya Alfajiri	2
2	Baada ya Salaa ya Adhuhuri	2
3	Baada ya Salaa ya Magharibi	2
4	Baada ya Salaa ya Isha	2
5	<i>Al-Witr</i> (baada ya Salaa ya Isha)	3

#### **Maelekezo:**

1. Salaa ya *Al-Witr* husaliwa baada ya Salaa ya Isha. Unaweza kuisali wakati wowote mpaka kabla ya kuingia wakati wa Salaa ya Alfajiri.
2. Salaa ya Ijumaa husaliwa badala ya Salaa ya Adhuhuri nayo ni lazima kwa kila mwanamume mkaazi. Kwa hivyo ukiikosa Salaa ya Ijumaa, ni lazima usali Adhuhuri. Wanawake, wasafiri na wagonjwa hawalazimiki kusali Salaa ya Ijumaa, (yaani anatakiwa asali Adhuhuri). Salaa ya Ijumaa huanzia kwa Khutba baadae husaliwa Raka'a mbili za Salaa ya Ijumaa. Haisaliwi isipokuwa katika jamaa, baadae hufuatia na Raka'a mbili au nne za Sunna.
3. Kuna namna nyingi za Salaa kwa mfano Tarawehe ya mwezi wa Ramadhan, Salaa za Idi mbili, Salaa ya maiti na kadhalika. Maelezo zaidi ya Salaa hizi yanaweza kupatikana katika vitabu vyta za Salaa.



## 2. Nyakati za Salaa

Salaa tano za faridha za kila siku lazima zisaliwe katika nyakati zake maalumu zilizowekewa.

Salaa ya Alfajiri ( <i>Fajr</i> )	Kutokea kuingia alfajiri mpaka kufikia kuchomoza juu.
Salaa ya Adhuhuri ( <i>Dhuhur</i> )	Mchana baada ya juwa kupindukia upande wa magharibi, mpaka inapoingia Alasiri.
Salaa ya Alasiri ( <i>Asr</i> )	Pale kivuli cha kitu kinapo kuwa sawa na urefu wake, mpaka kabla ya kutuwa juwa.
Salaa ya Magharibi ( <i>Maghribi</i> )	Baada ya kutuwa juwa mpaka kupotea wekundu wa juwa.
Salaa ya Isha ( <i>Isha</i> )	Baada ya kupotea wekundu wa juwa mpaka nusu ya usiku.

Nyakati za Salaa huandikwa katika misikiti yote. Vilevile unaweza kuzipata katika simu za mikononi za kisasa, ambazo zinakupa nyakati za Salaa za dunia nzima.

Zifwatazo ni nyakati amabazo Salaa hairuhusiwi:

1. Pale linapochomoza juwa mpaka litoke kamili.
2. Pale juwa linapokuwa utosini, mpaka lipindukie upande wa magharibi.
3. Pale linapotuwa juwa mpaka lipotee kabisa.

Vilevile Salaa hazisihi katika hali zifuatazo:

- a. Baada ya kusali Salaa ya Alfajiri, mpaka lichomoze juwa kamili, (isipokuwa Salaa za lazima kama Salaa ya maiti).
- b. Baada ya kusali Salaa ya Alasiri mpaka lituwe juwa (isipokuwa Salaa za lazima kama Salaa ya maiti).



### **3. Vipi kusali.**

Utaratibu wa kusali Salaa za faridha tano za kila siku na Salaa za *Sunna* umeelezewa katika Mlango wa Tisa. Salaa zote husaliwa kwa kuelekea *Ka'abah* huko Makkah. Kuelekea huku kunaitwa *Qiblah*. Unaweza kupata uwelekezi wa *Qiblah* pahala opote duniani katika simu za mkononi za kisasa.

### **4. Vitendo vinavyo haribu Salaa.**

Kuna namna mbili za vitendo vinavyo haribu Salaa; (a) vitendo vinavyo husiana na hali ya akili, yaani hali ya undani wa moyo, (b) vitendo vya harakati.

#### **A. Vitendo vinavyo husiana na hali ya akili.**

1. Kubadilisha niya kati ya Salaa. Kwa mfano kubadilisha badala ya Salaa ya *faridha* ukasali Salaa ya *Sunna*.
2. Kupotewa na fahamu kwa kusinzia au kuzimia. Kwani shuruti ya Salaa inatakiwa akili yako iwe timamu wakati wa kusali.
3. Kuishughulisha sana akili yako kwa mambo yasiyohusu Salaa.



## B. Vitendo vya harakati

1. Kuwacha mambo muhimu yafuatayo:
  - a. Kutia niya (*Niyya*)
  - b. Kusimama (*Qiyam*)
  - c. *Takbiratul Ihram* (kusema *Allahu Akbar* wakati wa kuanza Salaa)
  - d. Kuwa na moyo ulio dhibiti bila ya fikra za nje ya kitendo chako cha Salaa (yaani *Khushu'u*)
  - e. Kusoma *Suratul Fatiha* (Alhamdu) katika Raka'a zote.
  - f. Kuinama (*Rukuu*)
  - g. Kusujudu (*Sujud*)
  - h. Kukaa (*Tashahhud*)
- i. *At-Taslim* (kusema *Assalamu alaykum wa rahmatul Llah mwisho wa Salaa*)
2. Kula au kunywa ndani ya Salaa.
3. Kuzungumza (kusema) chochote kisichohusu Salaa.
4. Kutabasamu (kusudi) au kucheka kwa sauti.
5. Harakati za kila mara ambazo hazimo katika Salaa.
6. Chochote kinacho tenguwa *Wudhuu*.



## Mlango wa 5 - Salaa ya jamaa

(Soma mlango huu baada ya kumaliza kusoma Mlango wa Nne na Mlango wa Tisa)

### A. Tofauti baina ya Salaa ya jamaa na ile ya mtu peke yake:

1. Unaposali peke yako unatakiwa kuqimu Salaa (*Iqama*), kama ilivyo elezewa katika Mlango wa Tisa. Katika Salaa ya jamaa, yule aliyeaadhini ndiye anayeqimu kwa wote. (Wanawake hawatakiwi kuqimu Salaa).
2. Unapokuwa unasali peke yako, kila unachokisoma kinakuwa kimya (yaana hutowi sauti). Lakini unapokuwa uansali jamaa utamsikia Imamu anasema kwa sauti haya yafuatayo:
  - a. *Allahu Akbar* (*Takbiratul Ihram*), mwanzo wa Salaa.
  - b. Kusoma sura ya *Alfatiha* katika *Raka'a* mbili za mwanzo. (isipo kuwa Salaa ya Adhuhuri na Alasiri kwani hizi husomwa kimya).
  - c. Kusoma Sura baada ya *Alfatiha* katika *Raka'a* mbili za mwanzo, (kwa zile Salaa zinazotakiwa kusomwa sura).
  - d. '*Allahu Akbar*' anapo inama (*Ruku'u*), kusujudu, kukaa na kusimama.
  - e. *Samia' Llahu Liman Hamida* anapoinuka Imamu baada ya *Ruku'u*.
  - f. '*Salaamu Alaykum Warahmatullah*' anapomaliza Imamu Salaa.

Wewe unayesali nyuma ya Imamu utarudia kimya yale anayo yasoma Imamu isipokuwa anaposoma Sura (nukta 'c') wewe unakuwa unasiliza, na (nukta 'e') wewe utasema *Rabbana Walakal Hamd* baada ya kunyanya.

3. Unapo kuwa unasali peke yako utasoma kimya *Alfatiha* na Sura (katika



Salaa zinazohitajiwa kusomwa Sura). Lakini katika Salaa ya jamaa utasoma *Alfatihha* kimya (nyuma ya Imamu bila ya kumkiyuka) na utakuwa unamsikiliza Imamu pale anaposoma Sura.

## B. Namna ya kuingia katika Salaa ya jamaa.

Ikiwa umekuja katika Salaa ya jamaa nawe umechelewa na Salaa inasaliwa, unaweza kuunga hiyo jamaa na baadae ukakamilisha yaliyo kupita anapo maliza Imamu na kusema *Salaamu Alaykum wa Rahmatullah*. Ifwatayo ni mifano miwili ya kuunga Salaa ya jamaa.

### Mfano wa Kwanza

Katika Salaa ya *Isha* umemkuta Imamu anasoma *AlFatihha* katika *Raka'a* ya pili. Ingia katika Salaa kwa namna hivi ifuatavyo:

1. Soma *Tawjih*.
2. Toa *Takbiratul Ihraam*, ‘*Allahu Akbar*’.
3. Sema ‘*Audhu Billahi Mina Shaytani Rajim*.’
4. Soma *Alfatihha* kwa kumfuata Imamu.
5. Msikilize Imamu anapo soma Surah baada ya *Al-Fatiha*.
6. Mfuate Imamu mpaka mwisho wa Salaa.
7. Anapo maliza Imamu Salaa, nyanyuka bila ya kusema ‘*Allahu Akbar*’.
8. Soma *Alfatihha* na *Surah*.
9. Rukuu na usujudu tena uinuke.
10. Hapa unakuwa umefika pale ulipo ingia katika Salaa.
11. Rudi chini ukae bila ya kusema ‘*Allahu Akbar*’.
12. Maliza Salaa yako kwa kusema ‘*As-Salaamu Alykum Warahmatu'llah*’.

### Mfano wa Pili

Wakati wa Salaa ya Adhuhuri umemkuta Imamu yumo katika Tahiyatu ya kwanza. Unga Salaa kama ifuatavyo:



1. Soma *Tawjih*.
2. Toa Takbiratul Ihraam, ‘*Allahu Akbar*’.
3. Sema ‘*Audhu Billahi Mina Shaytani Rajim*.’
4. Kaa bila ya kusema *Allahu Akbar* na umfuate Imamu mpaka mwisho wa Salaa.
5. Pale anapo maliza Imamu Salaa inuka bila ya kusema ‘*Allahu Akbar*’
6. Soma *AlFatihah*, rukuu, sujudu na uinuke. (Hii ni *Raka'a* ya kwanza).
7. Soma *AlFatihah*, rukuu, sujudu na ukae. (Hii ni *Raka'a* ya pili).
8. Hapa unakuwa umefika pale ulipoingia katika Salaa.
9. Ikiwa uliwahi kusoma *Tahiyat* ya kwanza ulipounga Salaa, maliza Salaa yako kwa kusema *Assalamu Alaykum wa Rahmatul Lah*. Ikiwa hukuwahi basi soma *Tahiyat* ya kwanza na umalize Salaa yako.

Unaweza kuingia katika Salaa ya jamaa popote unapowahi halafu unalipa yaliyo kupita kwa njia hii tuliyo fahamisha katika mifano hii. Nukta muhimu ni kuendelea na Salaa pamoja na Imamu mpaka mwisho na kulipa yale yaliyo kupita.



## **Hadithi kuhusu Salaa ya jamaa**

قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ  
مَنْ صَلَّى الْعِشَاءَ فِي جَمَاعَةٍ فَكَانَمَا قَامَ نِصْفَ  
اللَّيْلِ وَمَنْ صَلَّى الصُّبْحَ فِي جَمَاعَةٍ فَكَانَمَا صَلَّى  
اللَّيْلَ كُلَّهُ

Mtume wa Allah amesema: Yeyote atakayesali Salaa ya Isha katika jamaa, ni kama aliyesali mpaka usiku wa manane, na yule atakayesali Salaa ya Alfajiri katika jamaa ni kama aliyesali usiku kucha.

*(Imeandikwa na Muslim na at-Tirmidhi)*

عَنْ عُثْمَانَ بْنِ عَفَّانَ، قَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى  
اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ « مَنْ تَوَضَّأَ لِلصَّلَاةِ فَأَسْبَغَ  
الْوُضُوءَ ثُمَّ مَشَى إِلَى الصَّلَاةِ الْمُكْتَوَبَةِ فَصَلَّاهَا  
مَعَ النَّاسِ أَوْ مَعَ الْجَمَاعَةِ أَوْ فِي الْمَسْجِدِ غَفَرَ اللَّهُ  
لَهُ ذُنُوبَهُ »

Imeelezewa kuwa Uthman ibn Affan amesema:

“Nilimsikia Mtume (saw) akisema: Yeyote atakayetia Wudhuu vizuri, akenda kwa miguu msikitini kuhudhuria Salaa ya faridha, akasali pamoja na watu katika jamaa au ndani ya msikiti, Allah atamsamehe madhambi yake.”

*(Imeandikwa na an-Nasa'i)*



## Mlango wa 6 - Mambo Yanayohusu Wanawake

Mambo yanayohusu *Tahara* na *Salaa* ambayo yanawahu su wanaume na wanawake yameshae lezewa katika sehemu mbalimbali za kitabu. Mlango huu unaelezea mambo yanayowahu su wanawake tu.

1. Wanawake hawatakiwi kusali wala kufunga wakati wa ada zao za mwezi na pia baada ya uzazi mpaka asafike.
2. Wanawake wanatakiwa wakoge ili kujitia *Tahara* mara tu wakiona alama za kumalizika damu ya *Hedhi* au *Nifaas*, hata ikiwa itakuwa kabla ya ule muda ambao wanasubiri kumalizika kutoka hiyo damu.
3. Mwanamke anaporejea katika hali ya *Tahara* hatakiwi kulipa zile *Salaa* zilizo mpita wakati alipokuwa katika *Hedhi* au *Nifaas*.
4. Kutokwa kwa damu ya *Hedhi* ni baina ya siku tatu mpaka kumi. Ikiwa itatoka kwa muda wa chini ya siku tatu, basi hiyo siyo *Hedhi*. Anatakiwa mtu akoge kujitia *Tahara* na kuendelea kusali. Vilevile anatakiwa azilipe zile *Salaa* zilizo mpita.
5. Muda wa *Hedhi* unatafautiana baina ya kila mwanamke. Siku huhesabiwa kutoka ile saa inapoanza kutoka damu mpaka saa ileile siku ya pili. Kwa mfano ikiwa damu itaanza kutoka saa tatu asubuhi, basi saa tatu asubuhi ya siku ya pili inahesabiwa kuwa ni siku moja.
6. Mwanamke anatakiwa kukoga na kurejea kufanya ibada zake mara tu akiona kuwa damu imesita na alama zake ni kukauka au kutokwa na urenda mweupe kama maziwa.
7. Ikiwa muda wa *Hedhi* utapindukia siku kumi au muda wa *Nifaas* utapindukia siku arubaini, anatakiwa mtu akoge kujitia *Tahara* na aendelee na ibada zake.
8. Wanawake ambao wanajuwa dasturi ya siku zao za ada ni ngapi wanatakiwa wasubiri siku mbili (masaa 48), ikiwa damu inaendelea kutoka, au siku moja (masaa 24) ikiwa urenda unaendelea kutoka, kabla ya kukoga. Kwa mfano, ikiwa mwanamke siku zake za ada ni sita, anatakiwa akoge baada ya kumalizika siku ya nane ikiwa damu inaendelea kutoka, au katika siku ya saba ikiwa urenda unaendelea kutoka. Kwa wale ambao siku zao



hazina dasturi, au kwa wale wanaoanza *Hedhi* basi wafuate kanuni ya siku kumi (tazama namba 7 hapo juu).

9. Kinachotoka kabla ya kuanza siku za *Hedhi* hakichukuliwi kuwa ni *Hedhi*.
10. Kinachotoka baada ya kusita damu ya *Hedhi* kinachukuliwa kuwa ni *Hedhi* kwa muda wa masaa 24. Katika muda huu wa masaa 24 ukiona alama za kumalizika *Hedhi* unatakiwa ukoge.
11. Damu wanayoipata watoto wadogo (chini ya miaka  $8 \frac{1}{2}$ ) na wale wanawake walio pindukia wakati wa kupata *Hedhi* haichukuliwi kuwa ni *Hedhi*. Hawana haja ya kukoga bali ni kujisafisha tu na kuendelea na Salaa zao.
12. Wanawake wanapotaka kukoga baada ya *Hedhi* au *Nifaas* wanatakiwa kuzifunguwa nywele zao ikiwa zimesukwa ili kuhakikisha zinakosheka vizuri na maji kufikia mpaka ngozi ya kichwa. Lakini pale anapokoga *Janaba* baada ya kitendo cha ndoa mtu hana haja ya kuzifunguwa nywele. Hakikisha tu kuwa maji yanafika kwenye ngozi ya kichwa.
13. Wanawake wanaweza kusali katika jamaa msikitini. Lakini Mtume (saw) kasema: “Salaa ya mwanamke ni bora zaidi nyumbani kwake”. Juu ya haya, akiwa atakwenda kusali jamaa anatakiwa kuvala mavazi yaliosawa bila ya urembo wowote.



## Mlango wa 7 - Tafauti katika Salaa baina ya Wanavyuoni wa Sheria za Kiislamu

Sharia za Kiislam, desturi na namna ya kuabudu zimetokana na Qur'an na mafunzo ya Mtume Muhammad (saw). Makundi mbalimbali ya ilimu yamefasiri hizi sharia kwa mujibu wa ilimu na fikra zao. Makundi haya, ambayo yanajulikana kama ni *Madhhabe*, hayatafautiani katika msingi asili wa sharia na desturi za kuabudu. Tafauti ziliyomo ni kidogo, zaidi katika kufasiri baadhi ya aya za Qur'an na mafunzo (*Hadithi*) za Mtume (saw).

Waislamu dunia nzima wanafuata maamrisho yaleyale ya Salaa tano za kila siku, na wanafuata shuruti asili za Salaa. Ingawaje kuna tafauti ndogo sana kuhusu Salaa na maamrisho yake. Zifuatazo ni baadhi ya khitilafu:

1. Kusema '*Bismillah*' unapotia *Wudhuu*.
2. Kunyanyuwa mikono juu unapoanza kusali unaposema *Takbiratul Ihram*, pia kabla na baada ya kurukuu.
3. Kusoma *Tawjih* kabla au baada ya *Takbiratul Ihram*.
4. Kufunga mikono kwenye kifuwa unapokuwa umesimama.
5. Kusoma baadhi ya aya za Qur'an baada ya *AlFatiha* katika *Raka'a* ya kwanza na ya pili za Salaa za Adhuhuri na Alasiri.
6. Kusoma dua katika Salaa, (*Qunut*).
7. Kusema *Aamin* baada ya Imamu kumaliza kusoma *Al-Fatiha*.

Tafauti hizi hazitengawi asili yenye we ya Salaa na masharti yake. Kitu muhimu ni kusimamisha Salaa za kila siku ili kufuata amri za Allah (swt) ili tuwe katika kumkumbuka na kumuogopa Allah. Ni busara kufuata kundi la watu wako ambalo linafuata mzizi ulio thabiti kutokana na Qur'an na mafunzo (*Hadithi*) ya Mtume (saw).



لَيْسَ الْبَرُّ أَنْ تُؤْلِمَا وُجُوهُكُمْ قَبْلَ الْمَشْرِقِ  
وَالْمَغْرِبِ وَلِكُنَّ الْبَرُّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ  
الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّنَ وَءَاتَى الْمَالَ  
عَلَى حُبِّهِ ذُو الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَأَبْنَى  
السَّبِيلَ وَالسَّاَبِلِينَ وَفِي الْرِّقَابِ وَأَقَامَ الْأَصَلَوَةَ  
وَءَاتَى الْزَّكَوَةَ وَالْمُؤْفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا  
وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَاسِيَاءِ وَالضَّرَاءِ وَحِينَ الْبَاسِ  
أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُنْقُونَ

*Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, (kuacha huru mtumwa) na akawa anashika Salaa, na akatoa Zakaa, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao. (Qur'an 2:177)*



## Mlango wa 8 - Mambo Mbalimbali na Dasturi

Yafuatayo ni mambo ambayo yanatakiwa kufuatwa katika kutekeleza Salaa na dasturi zake.

### Kuwa tayari kwa ajili ya Salaa

Maliza kazi zako zote muhimu, baadae nenda chooni umalize haja zako ili uwe katika hali ya kutokuwa na fikra. Kwani haya yatakusaidia kuwa umo katika hali ya unyenyekevu kamili wakati wa Salaa, kwani jambo muhimu katika Salaa ni unyenyekevu na utulivu. Allah (swt) anasema;

َقَدْ أَفَلَحَ الْمُؤْمِنُونَ \* الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَلِيلُونَ \*

*Hakika wamefaulu Waumini, ambao ni wanyenyekevu kaika  
Salaa zao. (Qur'an 23:1-2)*

### Kanuni za Mavazi

Allah (swt) ametuamrisha tuvae vizuri wakati tunapo sali;

يَبْنَىٰ عَادَمَ حُدُواً زِيَّنَتُكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ

*Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila Sala.  
(Qur'an 7:31)*

Nguo unayovaa inatakiwa ifunike sehemu zote za siri (*A'wrah*). Kwa wanaume, ingawa *A'wrah* ni ile sehemu baina ya kitovu na mpaka chini ya magoti, lakini unatakiwa uvae vizuri, kwa ajili ya heshima ya kumkabili Allah katika Salaa. Ama wanawake wanatakiwa kuufunika mwili wao mzima isipo kuwa sehemu ya uso na viganja vya mkono. Nguo zinazobana au nyepesi zenye kuonyesha mwili hazifai kwa mwanamume na mwanamke. Vilevile wanaume hawaruhusiwi kuвая hariri wala dhahabu wakati wowote ule.



## **Salaa ya Jamaa**

Ni lazima kwa wanaume kusali Salaa zao tano msikitini katika jamaa, isipokuwa kwa dharura fulani itakayomziwia mtu kwenda msikitini kama ugonjwa, hali ya hewa mbaya sana, kuogopea usalama wake na kadhalika. Amesema Mtume (saw): “Salaa katika jamaa inayo daraja ishirini na saba kulinganisha na ile ya mtu peke yake.”<sup>6</sup>

Si lazima kwa mwanamke kusali jamaa.

## **Salaa za Sunna**

Salaa za *Sunna* ni zile zinazosaliwa zaidi ya zile Salaa tano za *Faridha* za kila siku, ili kupata *thawabu* zaidi na kuwa karibu na Allah. Mbali ya zile tulizozitaja katika Mlango wa Nne, sehemu ya kwanza, zifuatazo ni baadhi ya hizo Salaa za *Sunna*.

- ▶ *Raka'a* mbili unapo ingia msikitini kabla ya kukaa. Sunna hii inaitwa *Tahiyyatul Masjid*.
- ▶ *Raka'a* mbili au nne baada ya kutoka juu, mpaka kabla ya adhuhuri. Sunna hii inaitwa *Dhuha*.
- ▶ *Raka'a* mbili au nne kabla ya Salaa ya *Isha*.
- ▶ *Raka'a* mbili au zaidi za usiku ziitwazo *Qiyamul Layl* au *Tahajjud*.

Salaa za Sunna husaliwa *Raka'a* mbili mbili. Unaweza kuzisali msikitini, nyumbani au popote pale. Ingawaje Mtume (saw) ameusia kuwa baadhi ya Sunna ziwe zinasaliwa nyumbani.

## **Salaa unapo kuwa umo Safarini**

Unapokuwa umo safarini, unatakiwa kuzifupisha zile Salaa za *Raka'a* nne za Adhuhuri, Alasiri na Isha ujisali *Raka'a* mbili. Ama Alfajiri na Magharibi hubaki kama zilivyo. Unapo fupisha Salaa hizo unazisali *Raka'a* mbili za mwanzo na kusoma *Tahiyyat* kamili.

6 Hadithi hii imeandikwa na ar-Rabi'i, Bukhari, Ibn Majah na wengineo.



Unaweza kuchanganya Salaa zilizo fupishwa za Adhuhuri na Alasiri, wakati wowote baina ya Adhuhuri na mpaka kabla ya kuingia Magharibi. Pia Salaa ya Magharibi pamoja na ile ya Isha iliyofupishwa. Unapochanganya Salaa hizi hupswi kusali Salaa za Sunna isipokuwa *Witr*.

Unapokuwa umo safarini hulazimiki kusali Salaa ya Ijumaa, kwa hivyo unasali *Dhuhr*.

### **Salaa ya Mgonjwa**

Yafuatayo ni mambo anayoruhusiwa mgonjwa, kwa mujibu wa hali ya ugonjwa wake:

1. Mgonjwa anaweza kufupisha na kuchanganya Salaa zake kama msafiri.
2. Anaweza *Kutayammam* ikiwa hawezi kutumia maji kutia *Wudhuu*.
3. Anaweza kusali naye amekaa au amelala, na akiwa hawezi kurukuu au kusujudu, anaweza kufanya harakati hizi kwa kichwa.
4. Ikiwa hawezi kufanya harakati zote hizi basi atafanya kwa kuharakisha macho.
5. Ikiwa haya yote hayawezekani basi atatoa *Takbeer (Allahu Akbar)* tano kwa kila Salaa ya *faridha*.
6. Na ikiwa haya yote hayawezekani, basi huyo mgonjwa hajalazimika kusali. Allah hatubebeshi mzigo zaidi ya uwezo watu.

### **Kukosa Salaa**

Muislamu anatakiwa awe muangalifu wa kutekeleza Salaa. Allah amewahadharisha katika Qur'an wale wanao puuza Salaa zao;

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ★ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ

*Basi, ole wao wano sali, ambao wanapuuza Salaa zao.*

*(Qur'an 107:4-5)*

Ingawaje, ikiwa mmoja wenu imempita Salaa kwa kughaflika au kwa kulala,



anatakiwa asali mara tu baada ya kukumbuka au kuamka katika usingizi.

### Kusahau Sehemu ya Salaa

Ikiwa umesahau sehemu ya Salaa (isipokuwa zile muhimu zinazotenguwa Salaa yote, ambazo zimetajwa katika Mlango wa Nne, 4 B, a), unatakiwa kusujudu (*Sujud as-Sahw*) unapo maliza Salaa yako na kutowa salamu, *Assalamu Alaykum wa RahmatuLLlah*.

### Kuomba Du'a baada ya Salaa

Unapomaliza Salaa, khasa zile Salaa tano za *Faridha*, ni uzuri kusoma *Du'a* kwa kusema:

► أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ 3  
► اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ، وَمِنْكَ السَّلَامُ، تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَلِ وَالْإِكْرَامِ  
► اللَّهُمَّ اعِنَا عَلَى ذِكْرِكَ، وَشُكْرِكَ، وَحُسْنِ عِبَادِكَ  
► اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌ كَرِيمٌ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنَّا  
► اللَّهُمَّ صَلِّ وَسَلِّمْ وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدَ  
► كَمَا صَلَّيْتَ وَسَلَّمْتَ وَبَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا  
► إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

- Astaghfiru Llah (x3)
- Allahumma anta Salaam, wa minka Ssalaam, Tabaarakta ya dha ljalali wa l-ikram
- Allahumma ainna ala dhikrika wa alaa shukrika wa alaa husni ibaadatika
- Allahumma innaka affuwun karimun tuhibbul afwa fa afu anna
- Allahumma ssali wassalim wa baarik ala sayyidna Muhammad, wa ala aali sayyidna Muhammad, kama sallayta wa sallamta wa barrakta ala sayyidna Ibrahim, wa ala aali sayyidna Ibrahim, fil aalamina innaka hamidun majeed
- Allah, nakuomba msamaha (unasema mara tatu)
- Ewe Mola, Wewe ndio Usalama na asili ya Salama, Umetukuka na



Kusifika Ufalme Wako.

- Ewe Mola, nisaidiye katika kukukumbuka, na kukushukuru, na kukuabudu kwa namna ilio bora.
- Ewe Mola, Wewe ndio Msamehevu, Karimu na mwenye kupenda kusamehe, tunakuomba utusamehe.
- Ewe Mola, rehema zako na amani yako iwe juu ya Muhammad na aila yake, kama rehema zako na amani yako ulizo mpa Ibrahim na aila yake ulimwenguni kote, kwani shukurani zote ni zako, na Wewe ndio Uliyotukuka.

Hapa tena utasoma dua zozote unazo taka ikiwa kwa Kiarabu au hata lugha uitakayo. Zimo dua nyingi katika Qur'an ambazo unaweza kuzisoma baada ya Salaa au wakati wowote. Ufwatayo ni mfano wa dua iliyoko mwisho wa sura ya pili ya Qur'an.

رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَأَعْفُ عَنَّا وَأَغْفِرْ لَنَا وَأَرْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلَنَا فَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ

**Rabbana laa tuakhidhna in nasina au akhta'na, Rabbana wala tahmil alayna isran kama hamaltahu ala lladhina min qablina, Rabbana wala tuhammilna maala taqata lana bih, wa a'fu anna, waghfir lana, warhamna, anta Mawlama fansurna 'ala Iqawmil kaafirin**

*Mola wetu! Usituchukulie tukikosea. Mola wetu! Usitubebeshe mzigo kama ulio wabebesha wale walio kuwa kabla yetu. Mola wetu! Usitutwike tusiyo yaweza, na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tuge ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri.*

*(Qur'an 2:286)*



فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ  
إِنَّمَا تَرَكَ الْأَوْصَابِينَ

*Basi mtegemee Mweneyezi Mungu; hakika wewe uko juu ya  
Haki iliyo wazi. (Qur'an 27:79)*



## Mlango wa 9 - Taratibu ya Salaa

Kurasa zifuatazo zinaonyesha hatuwa mbalimbali za namna ya kusali. Kila Salaa ina Raka'a maalumu, kama inavyoonesha katika orodha ifwatayo. (Hatuwa ya 1 mpaka ya 8 huwa ni *Raka'a* moja; tazama picha ukurasa wa 37 mpaka 40)

Salaa	Raka'a	Hatuwa
<i>Alfajiri</i>	2	1-16
<i>Adhuhuri</i>	4	1-14, 2-16
<i>Alasiri</i>	4	1-14, 2-16
<i>Magharibi</i>	3	1-14, 8-16
<i>Isha</i>	4	1-14, 2-16
<i>Salaa ya ijumaa</i>	2	1-16
<i>Sunna</i>	2	1-16
<i>Witr</i>	3	1-14, 8-16

Maelezo yafuatayo ni kwa yule anaye sali pekeyake. Tafauti unapo sali katika jamaa zimeelezwa Mlango wa Tano.

### Uwongozi katika hatuwa za Salaa:

**Hatuwa ya 1:** Hapana Iqamah kwa mwanamke katika Salaa zote, wala kwa mwanamume anapo sali katika jamaa.

**Salaa ya Alfajiri: (Raka'a mbili, hatuwa 1-16, vilevile angalia yafuatayo):-**

**Hatuwa ya 2:** Unapo sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 8:** Unapo sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 14:** Soma Tahiyat A na B kisha nenda hatuwa ya 15 na 16.



## **Salaa za Adhuhuri na Alasiri (kila moja Raka'a nne, hatuwa ya 1-14, 2-16 na uangalie yafuatayo):-**

**Hatuwa ya 14:** Soma *Tahiyat A* baadae inuka huku unasema *Allahu Akbar*, tena endelea kutoka hatuwa ya 2 mpaka 16. Unapokuwa kwenye hatuwa ya 14 mara ya pili soma *Tahiyat A* na B kisha nenda hatuwa ya 15 na 16.

## **Salaa ya Maghribi (Raka'a tatu, hatuwa ya 1-14, 8-16 na uangalie yafuatayo):-**

**Hatuwa ya 2:** Unapo Sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 8:** Unapo Sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 14:** Soma *Tahiyat A* baadae inuka huku unasema *Allahu Akbar*, baadae endelea kutoka hatuwa ya 8 mpaka 16, na mara hii soma *Al-Fatiha* tu kwenye hatuwa ya 8. Unapokuwa katika hatuwa ya 14 kwa mara ya pili soma *Tahiyat A* na B kisha nenda hatuwa ya 15 na 16.

## **Salaa ya Isha (Raka'a nne, hatuwa 1-14, 2-16 na uangalie yafuatayo):-**

**Hatuwa ya 2:** Unapo Sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 8:** Unapo Sali peke yako utasoma sura fupi (kama *An-Nas* au *Al-Ikhlas* au *Al-Asr*) baada ya kusoma *Al-Fatiha*.

**Hatuwa ya 14:** Soma *Tahiyat A* baadae inuka na huku unasema *Allahu Akbar*, baadae endelea kutoka hatuwa ya 2 mpaka 16. Unapokuwa katika hatuwa ya 14 kwa mara ya pili soma *Tahiyat A* na B kisha nenda hatuwa ya 15 na 16.

Salaa ya Ijumaa na Salaa za *Sunna* husaliwa kama Salaa ya Alfajiri. Salaa ya *Witri* husaliwa kama Salaa ya Magharibi isipokuwa ukifika hatuwa ya 8 kwa mara ya pili, utasoma Surah fupi baada ya kusoma *Al-Fatiha*.



Hatuwa  
**1**

### Kujitayarisha (Isti'daad)

Qimu Salaa \*

Soma ‘Tawjih’ \*

Sema: “Allahu Akbar”  
(*Mwenyezi Mungu ni  
Mkubwa*)

Sema: “Audhu Billahi Mina  
Shaytani Rrajiym”  
(*Najikinga kwako Allah na  
Shaytani aliye laaniwa*)

Hatuwa  
**2**

### Kusimama (Qiyaam)

سورة الفاتحة: Soma:

*Surah ‘Al-Fatiha’\**



Hatuwa  
**3**

### Kuinama (Rukuu)

Sema: ”سبحان رب العظيم“  
“Subhana Rabbiya l’Adhim”,  
Mara 3  
(*Mola wetu Uliyetakasika na  
Kutukuka*)



Unaporukuu, sema:  
“Allahu Akbar”

Hatuwa  
**4**

### Kuinuka (Qiyaam)

”ربنا و لك الحمد“  
“Rabbana walaka l’Hamd”  
(*Mola wetu shukurani zote ni  
zakoi*)



Unapoinuka sema:  
“Samia llahu liman hamida”  
*Mwenyezi Mungu anamsikiya anayemshukuru*

\* Angalia ukurasa wa 41 mpaka 44.



Hatuwa  
5

### Sujuud ya kwanza (Sujuud)

Sema: "سبحان ربى الأعلى" x3  
"Subhana Rabbiya l'A'ala"

Mara 3

(*Mola wetu Ulyietakasika na  
Ulio Juu Kabisa*)



Unapo kuja kusujudu sema:  
"Allahu Akbar"

Hatuwa  
6

### Kukaa (Juluus) Kaa kimya kwa muda wa sekunde 3 - 4.



Unapokuja kukaa sema:  
"Allahu Akbar"

Hatuwa  
7

### Sujuud ya pili. (Sujuud)

Sema: "سبحان ربى الأعلى" x3  
"Subhana Rabbiya l'Aala"

Mara 3

(*Mola wetu Ulyietakasika na  
Ulio Juu Kabisa*)



Unapokuja kusujudu sema:  
"Allahu Akbar."

Hakbang  
8

### Kusimama (Qiyaam)

Soma: سورة الفاتحة  
*Surah 'Al-Fatiha'*\*



Unapokuja kusimama sema:  
"Allahu Akbar"



Hatuwa  
**9**

### Kuinama (Rukuu)

Sema: سبحان ربى العظيم“ x3  
“*Subhana Rabbiya l'Adhim*”,  
Mara 3  
(*Mola wetu Uliyetakasika na  
Kutukuka*)



**Unaporukuu sema:**  
“Allahu Akbar”

Hatuwa  
**10**

### Kuinuka (Qiyaam)

Sema: ”ربنا ولك الحمد“  
“*Rabbana walaka l'Hamda*”  
(*Mola wetu shukurani zote  
ni zako*)



**Unapoinuka sema:**  
“*Samia llahu liman hamida*”

*Mwenyezi Mungu anamsikiya anayemshukuru*

Hatuwa  
**11**

### Sujuud ya kwanza (Sujuud)

Sema: ”سبحان ربى الأعلى“ x3  
“*Subhana Rabbiya l'A 'ala*”  
Mara 3  
(*Mola wetu Uliyetakasika na  
Ulio Juu Kabisa*)



**Unapokuja kusujudu sema:**  
“Allahu Akbar”

Hatuwa  
**12**

### Kukaa (Juluus)

Kaa kimya kwa muda wa  
sekunde 3 - 4.



**Unapokuja kukaa sema:**  
“Allahu Akbar”

\* Angalia ukurasa wa 41 mpaka 44.



Hatuwa  
**13**

### Sujuud ya pili (Sujuud)

Sema: "سبحان ربى الاعلى" x3  
"Subhana Rabbiya l'A'ala"  
Mara 3  
(*Mola wetu Uliyetakasika na Ullo Juu Kabisa*)



Unapo kuja kusujudu sema:  
"Allahu Akbar"

Hatuwa  
**14**

### Kukaa (Juluus)

Soma: التحيات  
"Tahiyat" \*



Unapo kuja kukaa sema:  
"Allahu Akbar"

Hatuwa  
**15**

### Kutowa Salaam

Geuza uso wako kuliya.  
Sema: السلام عليكم  
Assalam Alaykum  
(*Salama zikufikieni*)



Hatuwa  
**16**

### Kutowa Salaam

Geuza uso wako kushoto.  
Sema: ورحمة الله  
Wa Rahmatu Llah  
(*Pamoja na Rehma za Mwenyezi Mungu*)



\* Angalia ukurasa wa 41 mpaka 44.



## KUQIMU (SALAA)

الله أكْبَرُ (٤ مرات)  
أَشْهُدُ أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ (مرتين)  
أَشْهُدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ (مرتين)  
حَيٌّ عَلَى الصَّلَاةِ (مرتين)  
حَيٌّ عَلَى الْفَلَاحِ (مرتين)  
قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ (مرتين)  
الله أكْبَرُ الله أكْبَرُ ، لَا إِلَهَ إِلَّا الله

## TAWJIH (KUJIELEKEZA)

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ ، تَبَارَكَ  
اسْمُكَ ، وَتَعَالَى جَدُّكَ ، وَلَا إِلَهَ  
غَيْرُكَ ، إِنِّي وَجَهْتُ وَجْهِي ، لِلَّذِي  
فَطَرَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ، حَنِيفًا  
وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

Allahu Akbar, Allahu Akbar (2x)  
Ash'hadu an laa illaha illa Llah (2x)  
Ash'hadu anna Muhammadan  
rasulu Llah (2x)  
Hayya alas Salaa (2x)  
Hayya alal Falah (2x)  
Qad Qaamati Salaa (2x)  
Allahu Akbar, Allahu Akbar  
Laa illaha illa Llah.

Allah ni Mkubwa. (mara nne).  
Nashuhudia kuwa hapana mungu  
wa kuabudiwa isipokuwa Allah.  
(mara mbili).  
Nashuhudia kuwa Muhammad ni  
mjumbe wa Allah. (mara mbili).  
Njooni musali (mara mbili)  
Njooni kwenye uwokovu. (mara  
mbili).  
Salaa imewadia (mara mbili).  
Allah ni Mkubwa. (mara mbili).  
Hapana mungu wa kuabudiwa  
isipokuwa Allah.

Subhanaka Llahumma wa  
bihamdika , Tabaaraka  
ismuka, Wa taala jadduka  
Wala illaha ghayruka , Inni  
wajaahatu wajhiya Lilladhiy  
fatara ssamaawati wal'ardha  
hanifan wa ma'anina  
l'mushrikin

Ewe Mola Umetakasika  
na shukurani zote ni zako.  
Limebariki jina lako na Utukufu  
wako ni mkuu. Hapana mungu  
wa kuabudiwa isipokuwa  
Wewe. Naelekeza uso wangu  
kwa Yule aliye umba mbingu  
na ardhi, na najiepusha na kila  
dhana mbaya na kushuhudia  
dini ya haki, wala mimi si  
mshirikina.



## TAHIYAT A (SALAMU)

الثَّجَيْلَاتُ الْمُبَارَكَاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ  
الظَّبَيْلَاتُ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ  
وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلَامُ عَلَيْنَا  
وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنَّ  
لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ  
وَرَسُولُهُ

Attahiyaatu lmubarakaatu  
Lillahi wa ssalawaatu wa  
ttayyibaatu, Assalamu  
alayka ayyuha nnabiyyu wa  
rahmatu llahi wa barakatu  
Assalamu alayna wa alaa  
ibadi llahi ssaalihin ,  
Ash'hadu an la illaha illa  
Llah wa ash'hadu anna  
Muhammadan abduhu wa  
rasuluh.

Salamu zote zenye kheri, sala  
na matendo mazuri ni za Allah.  
Amani iwe juu yako ewe Nabii,  
na rehema na baraka, amani iwe  
juu yetu na juu ya waja wema  
wa Allah. Nashuhudia kuwa  
hapana mungu wa kuabudiwa  
isipokuwa Allah, na nashuhudia  
kuwa Muhammad ni Mtumwa  
na Mtume Wake.

## TAHIYAT B

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ  
مُحَمَّدٍ ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ  
وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى  
مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ ، كَمَا بَارَكْتَ  
عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ فِي  
الْعَالَمَيْنِ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَحِيدٌ . رَبَّنَا إَنْتَ  
فِي الدُّنْيَا حَسَنَةٌ وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةٌ  
وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ .

Allahumma ssalli ala  
Muhammad wa alaa aali  
Muhammad kama salayta  
ala Ibrahim wa alaa aali  
Ibrahim wa barik alaa  
Muhammad wa alaa aali  
Muhammad kama barakta  
alaa Ibrahim wa alaa aali  
Ibrahim fil alamina innaka  
hamidunmajiid. Rabana  
aatina fiddunya hasanatan,  
wa filakhirati hasanatan,  
wa qina adhaba nnaar

Ewe Allah! Msalie Muhammad,  
pamoja na familia ya  
Muhammad kama ulivyo msalia  
Ibrahim na familia ya Ibrahim,  
na mpe baraka Muhammad  
na familia ya Muhammad  
kama ulivyompa baraka  
Ibrahim na familia ya Ibrahim  
katika mataifa kwani Wewe  
ni mwenye kustahili sifa na  
utukufu. Ewe Mola tupe hapa  
duniani yaliyo mazuri, na tupe  
yaliyo mazuri huko akhera, na  
utuepushe na adhabu ya moto.



## SURAH AL-FATIHA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ \* الرَّحْمَنُ  
الرَّحِيمُ \* مَالِكُ يَوْمَ الدِّينِ \* إِيَّاكَ نَعْبُدُ  
وَإِيَّاكَ نَسْتَغْفِرُ \* أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ  
\* صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرَ  
الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ

Bismillahi Rahmani Rahim.  
Alhamdu lillahi Rabbi l'aalamin, Arrahmaani Rahim,  
Maaliki yaumidiin, Iyaaka na 'abudu wa iyaka nastaiin,  
Ihdina ssiratal mustaqiim,  
Ssiraatal ladhma an'amta alaihim, Ghayri l'maghduhu bi  
'alayhim wala dhaaliin

- (1) Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwgingi wa rehema mwenye kurehemu.
- (2) Kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote (3) Mwingi wa rehema mwenye kurehemu.
- (4) Mwenye kumiliki Siku ya Malipo (5) Wewe peke yako ndiye tunayekuabudu na wewe peke yako ndiye tunayekuomba msaada (6) Tuongoze njia ilio nyooka (7) Njiya ya wale ambao uliyowaneemesha, siyo ya wale waliyo kasirikiwa na wale waliyopotea.

## SURAH AN-NAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ \* مَلِكِ النَّاسِ \* إِلَهِ  
النَّاسِ \* مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ \*  
الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ \* مِنْ  
الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ

Bismillahi Rahmani Rahim  
qul audhu birabbi nnaas,  
Maliki nnaas, Ilahi nnaas,  
Minsharri Iwaswaasi  
Ikhannaas, Alladhi yuwaswisu  
fi suduuri nnaas, Mina Ijinnati  
wa nnaas

Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwgingi wa rehema mwenye kurehemu.

Sema: Ninajikinga kwa Mola wa wanaadamu (1) Mfalme wa wanaadamu (2) Mungu wa wanaadamu (3) Na shari ya wasiwasi wa Shetani, mwenye kurejea nyuma (4) Anayetia wasiwasi katika nyoyo za watu (5) Kutokana na majini na wanaadamu (6)



## SURAH AL-IKHLAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ \* اللَّهُ الصَّمَدُ \* لَمْ يَلِدْ  
وَلَمْ يُوْلَدْ \* وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ كُفُواً أَحَدٌ

Bismillahi Rahmani Rahim,  
qul huwa Llahu Ahad , Allahu  
    Ssamad, Lam yalid walam  
    yuulad, Walam yakun lahu  
        kufuhan Ahad

Kwa jina la Mwenyezi Mungu  
mwinci wa rehema mwenye  
kurehemu.

Sema: Yeye Mwenyezi  
Mungu ni Mmoja tu (1)  
Mwenyezi Mungu yeyetu  
ndiye anayestahiki kukusudiwa  
(*kwa kumuabudu, kumuomba  
na kumtegemea*) (2) Hakuzaa  
wala hakuzaaliwa (3) Wala hana  
anayefanana naye hata mmoja  
(4)

## SURAH AL-ASR

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالْعَصْرِ \* إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُضْرٍ \* إِلَّا  
الَّذِينَ ءامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّلَاتَ وَتَوَاصَّوْا  
بِالْحَقِّ وَتَوَاصَّوْا بِالصَّبْرِ

Bismillahi Rahmani Rahim,  
Wal 'Asr, Innal Insana lafy  
khusr, illal ladhina aamanu wa  
amilus salihaati, watawasaw  
bil haqqi, watawasaw bis sabr

Kwa jina la Mwenyezi Mungu  
mwinci wa rehema mwenye  
kurehemu.

Naapa kwa Zama! (1) Hakika  
binaadamu bila ya shaka yumo  
katika khasara (2) Isipokuwa  
wale walio amini na wakatenda  
mema, na wakausiana kwa  
haki, na wakausiana kusubiri  
(3)



## **Hadithi kuhusu faida za Salaa**

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ - صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - «إِذَا تَوَضَّأَ أَحَدُكُمْ فَأَحْسَنَ الْوُضُوءَ ثُمَّ أَتَى الْمَسْجِدَ لَا يَنْهَزُهُ إِلَّا الصَّلَاةُ لَا يُرِيدُ إِلَّا الصَّلَاةَ لَمْ يَخْطُطْ حَطْوَةً إِلَّا رَفَعَهُ اللَّهُ بِهَا دَرَجَةً وَحَطَّ عَنْهُ بِهَا حَطِيلَةً حَتَّى يَدْخُلَ الْمَسْجِدَ فَإِذَا دَخَلَ الْمَسْجِدَ كَانَ فِي صَلَاةٍ مَا كَانَتِ الصَّلَاةُ تَحِسْنُهُ» .

### **Imeelezewa kuwa Abu Hurairah kasema:**

“Mtume wa Allah amesema: Pale mmoja wenu anapotia Wudhuu kwa ukamilifu, akaja msikitini naye hana makusudio mengine isipokuwa Salaa, basi kila hatuwa moja Mwenyezi Mungu humpandisha daraja moja, na humuondoshea dhambi moja, mpaka anapo ingia msikitini. Anapo ingia msikitini anahisabiwa yumo katika hali ya Salaa ikiwa nia yake ni kusubiri Salaa”

**(Imeandikwa na Ibn Majah)**

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ «أَفْضَلُ الصِّيَامِ بَعْدَ شَهْرِ رَمَضَانَ شَهْرُ اللَّهِ الْمُحَرَّمُ وَإِنَّ أَفْضَلَ الصَّلَاةِ بَعْدَ الْمَعْرُوضَةِ صَلَاةٌ مِنَ اللَّيْلِ» .

### **Imeelezewa na Abu Hurairah:**

Kuwa Mtume (saw) amesema: Katika funga iliyo bora kabisa baada ya funga ya Ramadhani ni ile katika mwezi wa Allah wa Muharram (Mfungo nne). Na Salaa bora kabisa baada ya tano za faridha ni Salaa za usiku, (*Qiyamul Layl*).

**(Imeandikwa na Abu Dawud)**



# Mlango wa 10 - Orodha ya Maneno

<b>Al-Fatiha</b>	Sura ya kwanza katika Qur'an.
<b>Adhaan</b>	Muito wa Salaa.
<b>'Awrah</b>	Sehemu za siri za mwili.
<b>Dhuhr</b>	Salaa ya adhuhuri (mchana).
<b>Fajr</b>	Salaa ya alfajiri.
<b>Faridha</b>	Salaa za lazima, (au vitendo vyovoyote kitaka Uislamu vya lazima).
<b>Imam</b>	Mtu anayeongoza Salaa ya jamaa.
<b>Iqamah</b>	Mwito wa kuanza Salaa ya jamaa.
<b>Isha</b>	Salaa ya usiku, (isha).
<b>Ka'abah</b>	Jumba liliopo katika Masjid Al-Haraam huko Makkah, kwa dasturi hufunikwa guo jeusi.
<b>Khutbah</b>	Ni yale maneno ya kuwausia watu yanayotolewa na Imamu kabla ya Salaa siku ya Ijumaa, (au hata katika Salaa za Idi mbili).
<b>Maghrib</b>	Salaa ya magharibi baada ya kutuwa juwa.
<b>Muadhin</b>	Yule mtu anayeita watu kusali. (Adhaan)
<b>Najasa</b>	Uchafu unaoonekana kama damu, mkojo na kadhalika.




<b>Niyyah</b>	Makusudio katika moyo na akili ya kutenda jambo.
<b>Qiblah</b>	Upande wa Makkah (kwenye Ka'aba) ambapo Waislamu huelekea wanaposali.
<b>Raka'a</b>	Duru moja ya Salaa yenye harakati za kusimama, kusoma, kurukuu na kusujudu.
<b>Sunna</b>	Salaa ya nyongeza. (au kitendo chochote cha nyongeza katika Uislamu).
<b>Surah</b>	Mlango wowote katika Qur'an.
<b>Tahara</b>	Usafi wa kiibada.
<b>Tarawih</b>	Sunna zinazosaliwa baada ya Salaa ya Isha katika mwezi wa Ramadhani.
<b>Tayammum</b>	Kutia Wudhuu kwa kutumia vumbi la mchanga au udongo nadhifu badala ya maji.
<b>Witr</b>	Sunna ya rakaa moja au tatu inayo saliwa baada ya Salaa ya Isha.
<b>Wudhuu</b>	Kujisafisha viungo maalumu vya mwili kabla ya kusali.



# الصلوة

## باللغة السواحلية



مركز التعريف بالإسلام  
Islamic Information Center

Sultan Qaboos Grand Mosque, Muscat  
Sultanate of Oman